



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA
(Barua zote zilumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Simu: +255 687 047 147
+255 718 794 311

Namba ya Nukushi.

Barua pepe : ded.kyerwadc@kagera.go.tz

Kumb.Na.BA.744/23/20/87



S. L. P. 72,
KYERWA.

23 Agosti, 2023

TANGAZO LA KUPANGISHA VISIWA VYA OMWIZINGA (IZINGA NA NYAKAZINGA) NA FORONGO.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa anawatangazia Wafugaji wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa, wenye nia ya kuomba eneo la kufugia la Visiwa vya Omwizinga(Nyakazinga na Izinga), kwa ajili ya ufugaji bora wa ng'ombe na Forongo kwa ajili ya ufugaji wa nyuki. Visiwa hivi viko kusini mwa Nyanda za malisho ya mifugo za SIINA, jirani na Kitongoji cha Mitoma na vinapakana na nchi jirani ya Rwanda.

Visiwa vitatumika kwa ajili ya vikundi vya ufugaji wa kisasa ikiwa ni mashamba darasa ya mifugo, kwa wafugaji kwenye nyanda nyingine za malisho.

1.0 Visiwa kwa ajili ya ufugaji bora wa ng'ombe(Omwizinga)

1.1 Izinga

Kisiwa hiki kina ukubwa wa hekta 475. Kinapatikana katika longitudo E $030^{\circ} 38.76^{\circ}$ na Latitudo S $01^{\circ} 20.3^{\circ}$. mwinuko kutoka usawa wa bahari ni mita 1,294.Kuna malisho bora na ya kutosha ya mifugo na nyanda hizi za malisho ya mifugo zinaweza kuhimili ufugaji wa ng'ombe 317 kwa mwaka, bila ya kuharibu mazingira na bioanuwai.

1.2 Nyakazinga

Kisiwa hiki kina ukubwa wa hekta 94.Kinapatikana kwenye longitudo E $030^{\circ} 39.14^{\circ}$.na latitudo S $01^{\circ} 21.34^{\circ}$ Mwinuko kutoka usawa wa bahari ni mita 1,288. Kisiwa kinafaa kwa ufugaji wa mifugo kwa sababu kina malisho bora ya

kutosha. Uwezo wa nyanda za malisho kuhimili mifugo ni ng'ombe 63 bila ya kuharibu mazingira na bioanuwai.

2.0 Kisiwa cha Forongo.

Kisiwa kina ukubwa wa hekta 68.29. Kinapatikana kwenye longitudo E $030^{\circ} 38.09^{\circ}$ na latitudo S $01^{\circ} 22.32^{\circ}$. Mwinuko kutoka usawa wa bahari ni mita 1,291. Kisiwa hiki hakifai kwa ufugaji kwa mifugo kwani kina miti na mawe mengi. Kisiwa kinafaa kwa ufugaji wa nyuki.

3.0 Masharti ya waombaji

Waombaji wanatakiwa kuzingatia masharti yafuatayo:-

1. Kiwe ni kikundi cha wafugaji kilichosajiliwa rasmi.
2. Wafugaji katika kikundi husika wawe ni Watanzania.
3. Wafugaji katika kikundi wawe na kadi ya NIDA au Namba ya NIDA.
4. Wafugaji wawe na umri usiopungua miaka 18.
5. Waweze kutoa ushirikiano kwenye vyombo ya Usalama kwenye maeneo hayo pindi wanapohitajika.
6. Kikundi cha wafugaji kitaje kiasi cha malipo ya fedha kitakachotoa ikiwa ni kodi ya kupangisha ng'ombe mmoja kwa mwaka. Malipo haya yatatolewa kila mwanzo wa mwaka wa Serikali(Julai).
7. Mfugaji mmoja katika kikundi hataruhusiwa kumiliki ng'ombe zaidi ya 80 kwa mwaka.
8. Kikundi kijenge jengo la wachungaji lisilo la kudumu kwenye zizi kwa mujibu wa Mkataba wa upangaji.
9. Kikundi kiwe tayari kuchangia ujenzi wa kibanio cha kudumu ili kudhibiti ng'ombe wakati wa utoaji wa huduma mbalimbali kama chanjo za mifugo.
10. Hairuhusiwi kufanya shughuli nyingine za kibinadamu ndani ya eneo zaidi ya ufugaji kwa mujibu wa Mkataba.
11. Biashara ya mifugo itakayovunwa itafanywa kwenye minada ya mifugo Wilayani Kyerwa.
12. Mifugo itaingizwa na kutolewa kwenye kisiwa husika kwa kufuata Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo inayosimamia usafirishaji wa mifugo kutoka eneo moja kwenda eneo lingine.

13. Vikundi vyatufugaji vitakavyokidhi vigezo vyakupangishwa, vitajaza **Mkataba wa Upangishaji wa machunga ya kisiwa husika wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa.**
14. Waombaji wabainishe kisiwa/visiwa wanavyoomba kupangishwa kwenye maombi yao.
15. Ada ya kushughulikia maombi ya **SHS 30,000.00** isiyorejeshwa, iwekwe kwenye **Akaunti ya NMB Namba 31910003424 Kyerwa DC Miscellaneous Deposit Account.**
16. Maombi yaambatishwe na nakala ya cheti cha usajili wa kikundi, Orodha ya wanakikundi yenye Namba zao za NIDA na Stakabadhi ya malipo ya Ada ya Maombi (Ada ya kushughulikia maombi).

4.0 Namna ya kutuma maombi

Waombaji watatuma barua ya maombi kwa

Mkurungenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa S.L.P 72 Kyerwa.

Au barua pepe: ded.kyerwadc@kagera.go.tz

Mwisho wa Kutuma maombi ni tarehe 15/09/2023 saa 9.30 za alasiri.

Tangazo limetolewa na:-



Mayala P. Sengerema
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURU YA WILAYA
KYERWA**

*MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURU YA WILAYA
KYERWA*